# MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

Mkataba huu tumeuweka leo tarehe 18/10/2024.

KATI YA

AMINA MUSSA DIBWA wa simu namba 0656740620

(Ambaye kwa maana ya mkataba huu ataitwa "**Mpangishaji**")

NA

CBN PREMIER LOGISTICS COMPANY LTD wa simu namba 0717500600

(Ambaye kwa maana ya mkataba huu ataitwa "**Mpangaji**")

**Mpangishaji na Mpangaji wanakubaliana yafuatayo:**

1. Kwamba muda wa Upangishaji ni miezi 12 na utaanza tarehe 21/10/2024 na kuisha tarehe 21/02/2025
2. Kwamba upangaji huu ni kwa matumizi ya ofisi
3. Kwamba kodi ya upangishaji ya nyumba/chumba ni TZS 1,000,000/= kwa mwezi ambayo italipwa kwa mkupuo wa miezi 12
4. Kwamba kodi ya awali ya Shs 6,000,000/= italipwa wakati wa kusaini mkataba huu na kodi za awamu zingine zitakuwa zikilipwa kila baada ya miezi mitatu
5. Kwamba kama mpangaji hajalipa kodi baada ya siku 15 atawajibika kulipa riba ya 10% kwa mwezi kwa kila deni linalodaiwa
6. Kwamba mpangaji atawajibika na ukarabati kwa uharibifu utakaosababishwa na yeye au jamiiyake.
7. Kwamba endapo ukarabati utaadhiri sura na ramani ya awali ya nyumba/chumba basi mpangaji ni lazima apate kibali na maelekezo ya kimaandishi kutoka kwa Mpangishaji

Sahihi za Mpangishaji [signature] na Mpangaji [signature]

Scanned with CamScanner

8. Kwamba mpangaji atagharamia ukarabati wowote utakaofanyika ambao haukuwa kwenyemakubaliano ya awali ya upangaji.
9. Kwamba mpangaji atawajibika na kulipia huduma muhimu kama za maji safi na taka, ada zatakataka, ada za ulinzi na umeme nk.
10. Kwamba mpangishaji anayo mamlaka ya kuweka mfumo mzuri wa kuchangia huduma za majisafi na taka na umeme au kusitisha huduma hizo
11. Kwamba kama mpangaji katimiza masharti yote ya mkataba huu ikiwa ni pamoja na kulipa ada zote kwa wakati, mpangishaji au mwakilishi wake hatambugudhi mpangaji katika kipindi chote cha mkataba huu
12. Kwamba mpangaji atakabidhi nyumba kwa mpangishaji wake kama alivyopewa wakati wa kukabidhiwa nyumba na mpangishaji
13. Endapo Kutakuwepo na Mgogoro wowote, taratibu za Usuluhishi Itakuwa kama Ifuatavyo.
    a. Kwamba wahusika watakutana pamoja na kumaliza tofauti zao mezani
    b. Kwamba kama tofauti itakuwa bado haijaisha, kesi inatapelekwa kwa balozi wa nyumba kumi.
    c. Kwamba ikishindikana kwa balozi wa nyumba kumi mgogoro utapelekwa kwa mwenyekitiwa kitongoji/mtaa
    d. Kwamba ikishindikana kabisa kwenye kitongoji/mtaa, mhusika anayedhani hajatendewa hakianayo haki ya kupeleka mgogoro kwenye vyombo vya juu kwa usuluhishi zaidi.
14. Kubadilishwa au kuboreshwa kwa mkataba
    i. Kwamba mpangishaji anayo haki ya kubadili au kuboresha mkataba huu muda wowote kadrihali itakapolazimu ili kukidhi haja ya mabadiliko ya muda, sheria/masharti na uhitaji wa mpangaji na/au Mpangishaji kwa makubaliano ya pamoja
    ii. Kwamba endapo mabadiliko hayakumhusisha mpangaji, mkataba ukisha boreshwa utaanzakutumika kipindi cha mkataba unaofuata
15. **Kwamba notisi ya mabadiliko ya kodi** yatatolewa na Mpangishaji si chini ya siku 30 kablaya mkataba wa zamani kuisha



Scanned with CamScanner

**16. Kusitisha Mkataba**

a) Kwamba notisi ya kusitisha mkataba kwa mpangaji au Mpangishaji utafanywa kimaandishi sichini ya siku 30 kabla ya siku ya kukatisha mkataba au kabla ya mkataba uliopo kuisha.

b) Kwamba kama usitishwaji wa mkataba utafanywa na Mpangishaji kwa ridhaa yake mwenyewe, Mpangishaji atawajibika kurudisha pesa zote zilizobaki za mkataba pamoja nanotisi ya kimaandishi ya siku 30 bure.

c) Kwamba kama usitishwaji utafanywa na mpangaji kwa ridhaa yake mwenyewe, au kama usitishwaji utafanywa kwa sababu mpangaji kakiuka moja ya vipengele katika mkataba huu, kodi iliyolipwa haitarudishwa na kama mpangaji anadaiwa kitu chochote atawajibika kulipa kabla ya kuhama vinginevyo taratibu za kisheria za madai zitafuata mkondo wake

17. Sababu zitakazofanya mpangaji akatishiwe mkataba wake

i. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake kuwa mgomvi kwa wenzake hata baada ya kuonywabila mafanikio

ii. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake kuwa kero kwa wenzake hata baada ya kuonywa bilamafanikio

iii. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake kutumia vyombo vyenye kuhatarisha usalama wakena jamii yake, majirani au mali za watu na mazingira – hii haitaji kuonywa.

iv. Ikigundulika kuwa mpangaji au mmojawapo wa jamii yake anafanya mojawapo ya shughuli zifuatazo: Ugoni, ushoga, usagaji, umalaya, madawa ya kulevya, wizi, utapeli, mihadharati, kutoa taarifa za kufanikisha uhalifu wowote na shughuli yeyote iliyopigwa marufuku

v. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake kufanya shughuli yeyote inayoadhiri wengine kiuchumi au kiafya

vi. Kwamba mpangaji anachelewesha kodi mara kwa mara bila ridhaa ya Mpangishaji (kodi itahesabika imecheleweshwa kama itakuwa ikilipwa



Scanned with CamScanner

zaidi ya siku 30 ya tarehe halali ya kulipa)

vii. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake kusababisha uchafu wa kwake mwenyewe, jamii yake au mazingira ya nyumba

viii. Kubadili matumizi ya nyumba kinyume na mkataba huu bila idhini ya kimaandishi ya Mpangishaji

ix. Kutumia bila kuchangia au kuchelewesha mara kwa mara uchangiaji wa huduma kama majina umeme nk.

x. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake hashirikiani na wapangaji wenzake kwenye mamboya msingi kama vile usafi, usalama nk)

xi. Mpangaji au mmojawapo wa jamii yake atavunja mojawapo ya vipengele katika mkataba huu

18. Mkataba na Sheria za Nchi

*a)* Kwamba mkataba huu haukukusudiwa kwa vyovyote vile kupingana na sheria yeyote ya nchi, ikitokea moja ya vipengele Katika mkataba huu vinapingana na sheria yeyote ya nchi basi sheria hiyo ya nchi itachukuliwa kama sehemu ya mkataba huu dhidi ya kipengele husika.

19. Kuafiki Mkataba

*a)* Kwamba mkataba huu tumeuweka tarehe tajwa hapo juu hapa mtaa wa M/ Nyamala............. Kata ya Katika mji wa Dar-es-Salaam.

*b)* Kwamba tukiwa na akili zetu timamu, bila kulazimishwa au kushawishiwa na mtu yeyote tumeweka sahihi zetu kama ishara ya kuusoma, kuuelewa na kukubaliana na masharti yoteyaliyotajwa katika mkataba huu na kuahidi kutekeleza kwa moyo wote

*c)* Kwamba tunakubali kukabiliwa na adhabu zitakazoambatana na kukiuka moja ya vipengelekatika mkataba huu

Sahihi za Mpangishaji ....[signature]....................na Mpangaji ....[signature]..........

MPANGAJI

JINA CBN PREMIER LOGISTICS CO.LTD

SAHIHI [signature]

TAREHE 18/10/2024

SHAHIDI WA MPANGAJI

JINA JUMA MUSSA KALASE

SAHIHI [signature]

TAREHE 18/10/2024

MPANGISHAJI

JINA AMINA MUSSA DIBWA

SAHIHI [signature]

TAREHE 18 Oktoba 2024

SHAHIDI WA MPANGISHAJI

JINA JANETH MACHA

SAHIHI [signature]

TAREHE 18 Oktoba 2024